**RATIBA YA SIKU 21 ZA KUFUNGA NA KUOMBA (Tarehe 3 hadi 23 Juni 2024) – KANISA LA NAIROBI BAPTIST**

**MADA: "KESHENI MUOMBE."**

**Kifungu cha mada:** "*Kesheni muombe, msije mkaingia katika majaribu. Kwa maana roho i radhi lakini mwili ni dhaifu*." (**Mathayo 26:41)**

| Siku 1 (Jumatatu): Tufundishe kuomba | Siku 2 (Jumanne): Shukrani | Siku 3 (Jumatano): Kukua Kiroho |
|---|---|---|
| **Luka 11:1 -** *Siku moja, Yesu alikuwa mahali fulani akiomba. Alipomaliza, mmoja wa wanafunzi wake akamwambia, "Bwana, tafadhali tufundishe kuomba kama Yohana Mbatizaji alivyowafundisha wanafunzi wake."*<br><br>**Isaya 30:18 -** *Hata hivyo BWANA anatamani kutupatia neema, anainuka ili kuwaonyesha huruma. Kwa kuwa BWANA ni Mungu wa haki. Wamebarikiwa wote wanaomngojea yeye!*<br><br>**Wakolosai 4:2 -** *Dumuni katika maombi, mkikesha na kushukuru.*<br><br>● Omba kwamba Mungu atatupatia upendo upya wa kuwa pamoja naye kwa muda mwingi katika maombi muhimu, yaliyo na matarajio (Mat. 2:42).<br>● Omba kwamba Bwana Yesu atatufundisha zaidi kuhusu yeye mwenyewe na kuhusu maombi tunapomngojea.<br>● Omba kwamba tutamruhusu Mchungaji Mwema atuongoze tunapoomba, tukitanguliza mapenzi yake kuliko tamaa zetu.<br>● Omba kwamba Bwana Yesu atatupeleka kwenye ngazi mpya ya maombi wakati huu wa siku 21 za kufunga na kuomba.<br>● Ombea nguvu na uvumilivu tunapomngojea Bwana Yesu kwa siku 21 zijazo na kwamba tutafanywa upya na kuona upendo na huruma zake.<br>● Omba kwamba Mungu atatusaidia tuishi tukiamini zaidi kwamba anatawala, yupo nasi, na anaweza kujibu kwa nguvu tunapoomba. | **Zaburi 9:1 -** *Ee BWANA, nitakutukuza kwa moyo wangu wote, nitayasimulia matendo yako yote ya ajabu.*<br><br>**Zaburi 100:4 -** *Ingieni malangoni mwake kwa shukrani na katika nyua zake kwa kusifu, mshukuruni yeye na kulisifu jina lake.*<br><br>**Wafilipi 4:6-7 -** *Msifadhaike juu ya jambo lo lote; lakini katika kila jambo mjulisheni Mungu haja zenu, kwa kusali na kuomba pamoja na kushukuru. Na amani ya Mungu, ambayo inapita ufahamu wote, italinda mioyo yenu na nia zenu kwa Kristo Yesu.*<br><br>● Mshukuru Mungu kwa zawadi ya thamani ya wokovu kupitia Yesu Kristo.<br>● Mshukuru Mungu kwa muda wa maombi tuliyopewa na kwamba itahuisha ibada yetu na kutembea kwetu pamoja naye.<br>● Bwana Yesu asifiwe kwa ahadi ya amani tunapomtafuta katika maombi.<br>● Omba kwamba Bwana Yesu atafungua macho yetu kwa yote mema ambayo amefanya ndani yetu, kupitia kwetu, na yanayotuzunguka na umshukuru.<br>● Mshukuru Mungu kwa ajili ya familia zetu na uombe atusaidie kuona mema ndani yao.<br>● Mshukuru Mungu kwa uzima, afya njema, riziki, na uhifadhi (Zaburi 103:1-5, Zaburi 107:8-9). | **2 Petro 3:17-18 -** *Rafiki wapendwa, tayari mnajua kuhusu hili. Hivyo iweni waangalifu. Msiwaruhusu watu hawa waovu wakawaongoza kwenye upotevu kwa mabaya wanayofanya. Jichungeni msipoteze imani yenu iliyo imara. Lakini mkue katika neema na kumjua Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo. Utukufu ni wake, sasa na hata milele! Amina.*<br><br>**1 Wakorintho 9:27 -** *lakini nauimarisha mwili wangu na kuutawala, ili baada ya kuwahubiria wengine, mimi mwenyewe nisije nikakataliwa.*<br><br>● Omba ili tukue katika neema na maarifa ya Yesu Kristo.<br>● Omba kwamba Bwana Yesu atatufundisha kutulia daima na kutafuta uso wake na ushauri<br>● Omba kwamba Mungu atatusaidia kuimarisha miili yetu na kuua tabia ya kimwili.<br>● Omba kwamba moto wa Roho Mtakatifu wa kusafisha utafanya kazi katika maisha yetu ili tuwe vyombo anavyoweza kutumia.<br>● Omba ili tuwe macho ili tusianguke kutoka katika hali yetu salama.<br>● Omba kwamba tutakua katika kujifunza na kutumia Neno la Mungu maishani mwetu.<br>● Omba Mungu atusaidie kuwa na subira katika dhiki na kuvumilia ili tuwe wakomavu na watimilifu, bila kupungukiwa na kitu (Yakobo 1:4). |

| Siku 4 (Alhamisi): Vita za Kiroho | Siku 5 (Ijumaa): Maombi dhidi ya Hofu | Siku 6: Maisha ya Jamii/ Mahusiano |
|---|---|---|
| **1 Petro 5:8-10 -** *Kaeni macho. Kesheni, maana adui yenu Ibilisi, huzunguka- zunguka akinguruma kama simba, akitafuta mtu atakayemmeza. Mpingeni, mkiwa thabiti katika imani, mkifahamu kwamba ndugu zenu pote duniani wanapatwa na mateso hayo hayo. Na mkisha kuteseka kitambo kidogo, Mungu wa neema yote ambaye amewaita katika utukufu wake wa milele katika Kristo, yeye mwenyewe atawa kamilisheni na kuwathibitisha na kuwatia nguvu.*<br><br>**Waefeso 6:12** - *Kwa maana hatupambani na binadamu, bali tunapambana na tawala na mamlaka na nguvu za ulimwengu huu wa giza na majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho.*<br><br>● Omba Mungu afungue masikio yetu ili kusikia na kuelewa Neno lake na sauti ya Roho wake.<br>● Omba tuwe macho na wenye akili timamu katika safari ya imani na kwamba Bwana Yesu atafichua eneo lolote la maisha yetu ambalo halijasalimishwa kwake, ili tuweze kujisalimisha kwake kikamilifu.<br>● Omba Bwana Yesu afungue macho yetu kuona mashambulizi yoyote ya shetani na kutupa hekima na ujasiri wa kumpinga adui kupitia maombi.<br>● Omba Roho Mtakatifu atufundishe na kutuongoza kutumia Neno la Mungu kama silaha yenye nguvu, sio dhidi ya binadamu, bali dhidi ya ufalme wa giza.<br>● Mpinge shetani na utangaze ukweli, mamlaka, na ubwana wa Kristo juu ya maeneo yoyote ya maisha na huduma ambayo yanashambuliwa.<br>● Omba kwamba tutasimama imara katika imani, hata katika mateso, na kwamba Bwana ataleta urejesho. | **Ufunuo 1:17-18 -** *Nilipomwona, nilianguka miguuni pake kama mfu. Lakini yeye akaweka mkono wake wa kulia juu yangu akasema, "Usiogope. Mimi ni wa kwanza na wa mwisho. Mimi ni Yeye aliye hai; nili kufa na tazama, mimi ni hai milele na milele! Nami ninazo funguo za mauti na kuzimu.*<br><br>**1 Yohana 4:18** - *Upendo uliokamilika hufukuza woga wote....*<br><br>● Omba tukumbuke daima kwamba Bwana Yesu anatawala na anatekeleza kikamilifu mapenzi yake kuu.<br>● Omba tuwe na imani ya kuamini Mungu ndiye Aliye Hai, Alfa na Omega, na hivyo hatuhitaji kuogopa.<br>● Omba Mungu, wa Kwanza na wa Mwisho, atusaidie tusiogope hali zozote zinazotukabili kwa sasa.<br>● Taja na utupie mahangaiko yako yote, woga na mizigo yako kwa Bwana Yesu, ambaye anatupenda.<br>● Omba kwamba tutahisi mkono wa kuume wa Mungu wa faraja juu yetu.<br>● Kama waaminio katika Bwana Yesu kama Mwokozi, tuombe atusaidie tusiogope kufa au kuishi, au Siku ya Hukumu, lakini tujenge uhakikisho wa kukubaliwa milele na kikamilifu kwa njia ya Bwana Yesu, aliye na funguo za mauti na kuzimu.<br>● Omba kwamba, kama waamini waliotangulia mbele yetu, tuwe na ujasiri na kushinda woga wote, ili tuweze kufanya mambo makuu ambayo Mungu anatuitia. | **Waefeso 4:31-32 -** *Ondoeni kabisa chuki yote, ghadhabu, hasira, ugomvi na matusi, pamoja na kila aina ya uovu. Muwe wema na wenye mioyo ya upendo kati yenu, na kusameheana kama Mungu alivyowasamehe kwa ajili ya Kristo.*<br><br>**Zaburi 25:9 -** *Huwaongoza wanyenyekevu katika haki, naye huwafundisha njia yake.*<br><br>**1 Petro 5:6 -** *Basi, nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu wenye nguvu, ili wakati wake ufaao utakapotimia, awainue.*<br><br>● Ombea hekima na neema ya kuishi kwa haki katika ulimwengu huu uliovunjika kama Yesu alivyofanya.<br>● Omba kwamba Bwana Yesu atatujaza na wema, unyenyekevu, msamaha, upendo, na rehema kwa watu wanaotuzunguka.<br>● Omba Mungu, ambaye huwaongoza wanyenyekevu katika lililo sawa, aongoze jinsi tunavyohusiana na wengine.<br>● Omba kwamba tusijiweke katika upinzani na Mungu kwa njia ya kiburi, lakini badala yake tuchague kujinyenyekeza mbele zake.<br>● Omba Bwana Yesu atufahamishe na ashughulikie chochote mioyoni mwetu ambacho hakimpendezi, k.m., uchungu, kutosamehe, hasira, kashfa, maneno makali, kiburi, n.k.<br>● Omba Bwana Yesu atuwezeshe kutambua tunapokosea kwa mahusiano na wengine ili tutubu na kutafuta msamaha.<br>● Omba Mungu arejeshe mioyo yetu na pia atutumie kuwarejesha wengine. |

| Siku 7 (Jumapili): Ujirani Wetu | Siku 8: Familia Imara za Kiungu | Siku 9 (Jumanne): Wanaume Wacha Mungu |
|---|---|---|
| **Yeremia 29:7 -** *Pia tafuteni amani na mafanikio ya mji ambamo nimewapeleka uhamishoni. Mwombeni Bwana kwa ajili ya mji huo, kwa sababu ukistawi, ninyi pia mtastawi.*<br><br>**Mathayo 22:39b -** *Mpende jirani yako kama nafsi yako.*<br><br>● Toa shukrani kwa mambo ambayo ni mazuri katika ujirani unapoishi.<br>● Ombea uwepo wa Mungu, amani, neema, kibali, utoaji, na ulinzi wa familia katika ujirani wetu.<br>● Mwombe Bwana Yesu atuongoze jinsi ambavyo angependa tuhusike katika ujirani wetu.<br>● Omba kwamba Bwana Yesu atatutumia sisi na waumini wengine kueneza manukato yake katika ujirani wetu.<br>● Omba kwamba tutaimarisha ujirani wetu mbele za Bwana Yesu kwa uaminifu katika maombi.<br>● Mwombe Bwana Yesu atupe nafasi za kushiriki habari njema zake na wale walio katika ujirani wetu.<br>● Ombea amani, usalama, na mahusiano mazuri kati ya watu wa ujirani wetu.<br>● Omba kwamba ujirani wetu uwe salama na baraka kwa wote, hasa watoto, wazee, na walio hatarini.<br>● Ombea maswala/changamoto mbalimbali zilizo katika ujirani wetu.<br>● Ombea hekima, neema, na nguvu za Mungu kwa ajili ya viongozi wanaosimamia ujirani wetu, k.m., kamati za ujirani, viongozi wa jumuiya, viongozi wa kisiasa, viongozi wa makanisa, n.k. | **Zaburi 127:1 -** *BWANA asipoijenga nyumba, wajengao hufanya kazi bure. BWANA asipoulinda mji, walinzi wakesha bure.*<br><br>**Matendo 10:2 -** *Yeye alikuwa mcha Mungu pamoja na jamii yake yote. Alitoa msaada kwa ukarimu kwa watu na kumwomba Mungu mara kwa mara.*<br><br>● Salimisheni familia zetu kwa Bwana Yesu, ili azijenge ziwe familia zenye nguvu na za kumcha Mungu na zinazoeneza Manukato ya Kristo.<br>● Omba familia zetu ziwe wakfu kwa Bwana Yesu, katika upendo na kumcha Mungu.<br>● Ombea wanafamilia ambao hawamjui Bwana Yesu Kristo wapate kumjua kama Bwana na Mwokozi.<br>● Mshukuru Mungu kwa mambo mazuri katika familia zetu.<br>● Mwombe Mungu aunganishe familia kwa upendo wa kweli.<br>● Ombea changamoto ambazo zinaweza kuwa zinakabili familia zetu.<br>● Ombea neema, amani, na Mungu aingilie kati wanafamilia na familia zinazopitia nyakati ngumu sana, k.m., afya mbaya, mkazo wa kifedha, mkazo wa kihisia, ugonjwa wa akili, matatizo ya kimahusiano, uraibu, maisha mapotovu, n.k.<br>● Omba Mungu amimine Roho wake atiaye uzima ndani ya wanafamilia na familia hizi.<br>● Mwombe Mungu alete tumaini kwa wasio na tumaini na kwa mahusiano yaliyovunjika. | **Zaburi 1:1-2** *Heri mtu yule ambaye haendi katika shauri la watu waovu, wala hasimami katika njia ya wenye dhambi, au kuketi katika baraza la wenye mizaha. Bali huifurahia sheria ya Bwana, naye huitafakari hiyo sheria usiku na mchana.*<br>**1 Timotheo 2:8 -** *Kwa hiyo, nataka kila mahali wanaume wasali wakiinua mikono iliyotakaswa pasipo hasira wala mabishano.*<br><br>● Omba wanaume wa makusanyiko yote ya NBC na vituo vya misheni wawe waaminifu kwa maombi na hivyo kutiwa nguvu na tabia ya kimungu inayokataa hasira na mabishano.<br>● Omba wanaume hawa wamheshimu na kumwamini Bwana Yesu, watembee katika njia zake na kumtumikia, na kwamba Mungu atawasaidia kuwa kielelezo cha Kristo kila mahali.<br>● Omba wanaume wa makusanyiko yote ya NBC na vituo vya misheni waishi maisha yao kikamilifu katika nuru ya Kristo na wasiwe na dhambi za siri.<br>● Omba wanaume wajitolee kikamilifu kwa njia na kazi za Bwana Yesu, wakistahimili licha ya changamoto wanazokabiliana nazo.<br>● Omba Bwana Yesu awainue na kuwatia nguvu wanaume waliokatishwa tamaa na changamoto za maisha.<br>● Ombea ushirika wa wanaume wa makusanyiko yote ya NBC na vituo vya misheni ziwe mabaraza ya kuwatia wanaume moyo katika mapambano yao na kuwasaidia kukua katika kumjua Kristo.<br>● Omba wasipuuze ushirika bali waelewe umuhimu wake (Waebrania 10:25). |

## Siku 10 (Jumatano): Wanawake Wacha Mungu

**Matendo 16:13 -** *Tulikaa Filipi kwa siku chache na siku ya sabato tukaenda nje ya mji kando ya mto, mahali ambapo tulidhani pange faa kwa maombi. Tukakaa chini tukaongea na baadhi ya wanawake waliokuja pale mtoni.*
**Mithali 31:30-31 -** *Kujipamba ili kuvutia ni udanganyifu na uzuri unapita upesi, bali mwanamke anayemcha BWANA atasifiwa. Mpe thawabu anayostahili, nazo kazi zake nazimletee sifa kwenye lango la mji.*
**Mithali 14:1 -** *Mwanamke mwenye hekima huijenga nyumba yake….*

- Omba wanawake wa makusanyiko yote ya NBC na vituo vya misheni wawe waaminifu katika maombi na hivyo kutiwa nguvu na tabia ya kimungu inayokataa hasira na mabishano.
- Omba wanawake hawa wamheshimu na kumwamini Bwana Yesu, watembee katika njia zake, na kumtumikia, na kwamba Mungu atawasaidia kuwa kielelezo cha Kristo kila mahali.
- Omba wanawake wa makusanyiko yote ya NBC na vituo vya misheni waishi maisha kikamilifu katika mwanga wa Kristo na wasiwe na dhambi za siri.
- Omba Bwana Yesu awasaidie wanawake hawa kuwa na hekima na kujenga familia zao, na si kuziharibu.
- Omba Mungu awashe karama zao mbalimbali motoni ili zitumiwe naye popote atakapowaweka (familia, jamii, kanisa, n.k.).
- Ombea urejesho wa wanawake wanaokumbana na kiwewe kikubwa, changamoto, na hasara katika maisha yao.
- Omba Bwana Yesu ajenge, kuimarisha, na kutumia huduma za wanawake za makusanyiko ya NBC na vituo vya misheni kwa utukufu na kusudi la milele.

## Siku 11 (Alhamisi): Watoto Wacha Mungu

**Mathayo 19:14 -** *Yesu akawaambia, “Waacheni watoto waje kwangu, msiwazuie; kwa maana Ufalme wa mbinguni ni wa walio kama hawa.*
**Malaki 2:15a -** *Je, Bwana hakuwafanya wao kuwa mmoja? Katika mwili na katika roho wao ni wa Mungu. Kwa nini wawe mmoja? Kwa sababu Mungu alikuwa akitafuta mzao mwenye kumcha Mungu.*

- Omba kusiwe na vizuizi kwa watoto kuja kwa Kristo katika kusanyiko lolote la NBC au kituo cha misheni.
- Ombea watoto katika makusanyiko yote ya NBC na vituo vya misheni wapate kumjua Bwana Yesu wakiwa wadogo na wasiache njia zake.
- Omba wazazi/walezi na wanafamilia wawe kielelezo cha Kristo na kuwafundisha watoto maadili ya kimungu kimakusudi.
- Omba Neno la Mungu litengeneze maisha ya watoto ili wamche na kumwamini Bwana Yesu, watembee kwa njia zake na kumtumikia na Mungu awasaidie kuwa kielelezo cha Kristo popote anapowaweka.
- Ombea kifuniko na ulinzi juu ya watoto wote katika nyakati hizi mbaya.
- Omba kwamba wachungaji wa huduma ya Watoto na walimu wa Sunday School wataathiri vizazi kumjua Bwana Yesu.
- Ombea shughuli za huduma ya Watoto, Sunday School, klabu ya Biblia ya Likizo, PPI shuleni, kambini, n.k., ivute wengi kwa Kristo.

## Siku 12 (Ijumaa): Vijana Wacha Mungu

**Zaburi 119:9 -** *Kijana aifanye njia yake kuwa safi jinsi gani? Ni kwa kutii akilifuata neno lako.*
**1 Yohana 2:14b -** *Ninawaandikieni ninyi akina baba, kwa kuwa mmemjua yeye aliyekuwapo tangu mwanzo. Ninawaandikieni ninyi vijana kwa sababu mna nguvu na neno la Mungu linakaa ndani yenu, nanyi mmemshinda yule mwovu.*

- Omba vijana wa makusanyiko yote ya NBC na vituo vya misheni wawe waaminifu katika maombi na hivyo kutiwa nguvu na tabia ya kimungu inayokataa hasira na mabishano.
- Omba vijana hawa wamheshimu na kumwamini Bwana Yesu, watembee katika njia zake, na kumtumikia, na Mungu awasaidie kuwa kielelezo cha Kristo.
- Omba vijana wa makusanyiko yote ya NBC na vituo vya misheni waishi maisha yao kikamilifu katika mwanga wa Kristo na wasiwe na dhambi za siri.
- Omba Mungu awalete vijana wasiomjua Kristo Yesu kwenye imani ndani yake.
- Omba Neno la Mungu liishi katika vijana ili watembee katika hofu ya Mungu, washike njia zao safi, wamshinde yule mwovu, na wasikubali kushindwa na majaribu yanayowazunguka.
- Ombea ukombozi kwa ajili ya vijana walio katika utumwa wa uovu wa aina yoyote, na kwamba wasitumike kueneza vurugu na kushiriki katika vitendo vya uhalifu, bali wajenge maisha yao, familia, kanisa na taifa.
- Omba Bwana Yesu atumie wachungaji na shughuli za huduma ya Vijana kuvuta vijana.

| Siku 13 (Jumamosi): Wahudumu Wacha Mungu | Siku 14: NBC Westlands & Kibra | Siku 15: NBC Kitengela & Ong'ata Rongai |
|---|---|---|
| **Waefeso 4:11-13 -** *Yeye ndiye aliyewapa watu vipawa, wengine kuwa mitume, wengine kuwa manabii, wengine kuwa wainjilisti, na wengine kuwa wachungaji na walimu; wapate kuwatayarisha watu wa Mungu kwa kazi za huduma, kwa ajili ya kujenga kanisa, ambalo ni mwili wa Kristo. Kazi hiyo itaendelea mpaka sote tuufikie umoja katika imani na katika kumjua Mwana wa Mungu; tupate kuwa watu waliokomaa kiroho kwa kufikia kiwango cha ukamilifu wote ulio ndani ya Kristo.*<br>**1 Petro 5:1-3 -** *Ninawasihi wazee waliomo miongoni mwenu, nikiwa mzee mwenzenu na shahidi wa mateso ya Kristo na mshiriki katika utukufu utakaofunuliwa. Lichungeni kundi la Mungu mlilokabidhiwa, si kwa kulazimishwa bali kwa hiari, si kwa tamaa ya fedha bali kwa moyo wenu wote. Msijifanye mabwana wakubwa kwa wale mnaowachunga bali muwe vielelezo kwa kundi hilo.*<br>● Omba Bwana Yesu awachunge aliowaita kuchunga wengine na kwamba atawatia mafuta na kuwapa neema na hekima ili kuwatayarisha watu wake kwa ajili ya kazi za huduma.<br>● Omba wawe wanyenyekevu, waaminifu, waliojitoa kwa Kristo, wenye bidii, waaminifu, waliotosheka katika utumishi kwa Kristo kama vielelezo.<br>● Omba Bwana Yesu awabariki wachungaji kwa pumziko kila upande na kulinda mioyo na akili zao ndani yake wanapohudumu katika shamba lake.<br>● Ombea riziki ya kimungu, na ulinzi dhidi ya yule mwovu kwa ajili yao na familia zao, ili wasiwe kwenye mtego wa dhambi na woga wa wanadamu.<br>● Omba Mungu afungue njia ya wale aliowaita kuchunga wengine ili kutekeleza mipango yake licha ya changamoto zozote. | **Yohana 17:3 -** *Na huu ndio uzima wa milele: wakufahamu wewe ambaye pekee ni Mungu wa kweli, na kumfahamu Yesu Kristo ambaye umemtuma.*<br><br>**NBC WESTLANDS**<br>● Shukuru Mungu kwa huduma za Watoto na Vijana.<br>● Ombea matendo ya Mungu na wafanyakazi wenza zaidi.<br>● Ombea mwongozo wa Mungu kwa mipango ya uchungaji, ya kusanyiko, na ya kitaasisi ambayo iko katika mchakato.<br>● Ombea wagonjwa na ushukuru kwa ajili ya wale walioruhusiwa kutoka hospitalini.<br>● Ombea upendeleo, uimarishwaji na ushirikiano katika mipango ya huduma zinazoendelea katika shule za msingi na sekondari za Farasi Lane, UON Lower Kabete, na chuo cha Matibabu Chiromo.<br>● Ombea mpito kuelekea ardhi ya Ngecha.<br><br>**NBC KIBRA**<br>● Mshukuru Mungu kwa ajili ya watu 101 (vijana na wazee) waliookoka kupitia shughuli mbalimbali za huduma.<br>● Omba watu wakue katika ujuzi na uhusiano wao na Mungu.<br>● Ombea nguvu za Mungu zionekane katika huduma zote za NBC Kibra.<br>● Omba watu wasihudhurie tu kanisani au kujitambulisha tu na NBC, bali wawe wa makusudi katika kumjua Mungu, na katika kukuza uhusiano wao na Mungu. | **Waefeso 3:16-17a -** *Namwomba Mungu awaimarishe kwa kuwatia nguvu mioyoni mwenu kwa njia ya Roho wake kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake. Na naomba kwamba, kwa imani, Kristo aendelee kuishi ndani ya mioyo yenu...*<br><br>**NBC KITENGELA**<br>● Shukuru Mungu kwa ajili ya kampeni ya huduma ya wanawake na usafishaji wa mazingira; wengi walisikia injili na 2 wakatoa maisha yao kwa Kristo.<br>● Shukuru Mungu kwa watu 69 ambao wamejiandikisha kwa mafunzo ya 3i8.<br>● Ombea nguvu na utoaji kwa washiriki walioathiriwa na mafuriko.<br>● Ombea faraja wale waliopoteza wapendwa wao na kwamba Bwana Yesu atazuia mkono wa kifo.<br>● Ombea washiriki wa timu za huduma wajazwe na kutiwa nguvu na Roho Mtakatifu.<br><br>**NBC ONG'ATA RONGAI**<br>● Omba kwa ajili ya maandalizi ya kimungu na nyenzo za kumaliza mradi wa ujenzi wa madarasa ya Sunday School.<br>● Ombea ukuaji wa kiroho na kufanywa upya na kwamba kila mshiriki ataimarishwa katika imani yake.<br>● Ombea neema ya Mungu na uwezeshaji wa huduma mbalimbali (Ibada, Watoto, Vijana, maombezi, Ufikiaji, Wanaume, na Wanawake, nk).<br>● Omba kwamba Bwana Yesu atabariki familia katika kusanyiko kwa umoja na upendo. |

| Siku 16 (Jumanne): NBC Kikuyu & Ngong’ Road | Siku 17: Viwanja vya Misheni vya Mitaa | Siku 18: Viwanja vya Misheni Duniani |
| --- | --- | --- |
| **Wafilipi 4:19-20 -** *Na Mungu wangu atawapeni ninyi kila kitu mnachohitaji kwa kadiri ya utajiri wake mtukufu katika Kristo Yesu. Mungu wetu na Baba yetu apewe utukufu milele na milele. Amina.*<br><br>**NBC KIKUYU**<br>• Mshukuru Mungu kwa ajili ya ukuzi wa nambari ya washirika katika kusanyiko.<br>• Ombea wokovu na ukuaji wa kiroho wa wote.<br>• Toa shukrani na omba kwa ajili ya uteuzi wa Mchungaji Kiongozi mpya (Pastor Elijah Mokaya).<br>• Ombea wahudumu zaidi na neema na nguvu za kuhudumu, hasa katika Sunday School na Outreach.<br>• Ombea ukuaji na athari za mipango ya uenezaji wa kusanyiko (shule na huduma ya chuo).<br>• Omba kwa ajili ya mradi wa kutengeneza lami wa Cabro na vifaa vya kanisa.<br><br>**NBC NGONG’ ROAD**<br>• Mshukuru Mungu kwa ajili ya wote waliookoka mwaka huu na kwa yote ambayo amefanya kupitia huduma mbalimbali.<br>• Ombea neema ya Mungu na kuwezesha huduma mbalimbali; kufikia shule na magereza, Easter Cantata, klabu ya Biblia ya Likizo, tamasha, Athari, Wanaume, Wanawake, Vijana, HGF, n.k.<br>• Omba kwa ajili ya kutiwa nguvu na uongozi wa Roho Mtakatifu kwa washiriki wote wa timu za huduma.<br>• Ombea wahudumu zaidi huku kusanyiko likitarajia kuanza ibada ya pili ya Jumapili.<br>• Omba kwa ajili ya maandalizi ya kimungu kwa mfumo mpya wa sauti. | **Matendo 1:8 -** *Lakini mtapokea nguvu akishawajilia Roho Mtakatifu, nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu na Yudea yote na Samaria, hadi mwisho wa dunia.*<br><br>• Toa shukrani kwa wale ambao wametoa maisha yao kwa Kristo wakati wa huduma mbalimbali za NBC na shughuli za huduma.<br>• Omba jina la Bwana Yesu litukuzwe sana ndani na kupitia makusanyiko yote ya NBC na vituo vya misheni.<br>• Omba Roho Mtakatifu awahukumu wale tunaohudumia lakini bado hawajasalimisha kwa Kristo ili awalete kwenye wokovu.<br>• Ombea misheni zote ambazo makusanyiko ya NBC na vituo vya misheni vinashiriki, k.m. shule, vyuo vikuu, magereza, uinjilisti wa mlango kwa mlango, ujirani, n.k.<br>• Omba makusanyiko yote ya NBC na vituo vya misheni viendelee kuwa mwanga wa Kristo Yesu.<br>• Ombea shughuli za kimmisionari za ustawi wa jamii za makusanyiko yote ya NBC na vituo vya misheni, k.m. kulisha wenye njaa, mpango wa wasomi wa Bapo, nk.<br>• Omba kwamba wengi watasikia injili kupitia misheni ya makusanyiko yote ya NBC na vituo vya misheni na kwamba watasalimisha maisha yao kwa Kristo.<br>• Omba kwamba, kupitia shughuli za misheni za mwezi wa mkazo wa umisheni wa Septemba, wengi watakutana na Mungu Aliye Hai. | **Zacharia 8:23 -** *Hili ndilo asemalo* BWANA *Mwenye Nguvu Zote: Katika siku hizo watu kumi kutoka lugha zote na mataifa, watang’ang’ania upindo wa joho la Myahudi mmoja na kusema, ‘Twende pamoja nawe kwa sababu tumesikia kwamba Mungu yu pamoja nawe.*<br><br>• Ombea misheni yetu ya *Kuenda Magharibi* na wamisionari huko, kwamba Mungu atawalinda wao na familia zao na kuwaandalia mahitaji yao ya kimwili, kijamii, kihisia na kiroho.<br>• Omba Mungu aendelee kuongoza NBC tunapoanzisha kituo cha misheni Afrika Magharibi na kwamba Mungu ataifanya imara nchi ambayo kituo hicho kiko.<br>• Mshukuru Bwana kwa matunda ambayo tayari anazaa watu (vijana na wazee) wanaposikia injili na wengine wamemjua Kristo Yesu kama Bwana na Mwokozi.<br>• Omba Mungu aweke mzigo mioyoni mwa watu wake kutumikia kama wamisionari wa muda mfupi na muda mrefu katika nyadhifa mbalimbali katika Afrika Magharibi.<br>• Ombea neema ya Mungu, rehema, ulinzi, na ukombozi kwa ajili ya Wakristo wanaoteswa katika Afrika Magharibi.<br>• Omba Mungu awape wamisionari na fedha kwa ajili ya misheni ya muda mfupi inayotarajiwa kwenda Bujumbura, Burundi baadaye mwaka huu.<br>• Ombea matunda zaidi yatakayodumu huku NBC ikiendelea na mpango wa misheni ya *Kuenda Magharibi*. |

| Siku 19 (Ijumaa): Toba na Uponyaji wa Kitaifa | Siku 20 (Jumamosi): Taifa la Kenya | Siku 21 (Jumapili): Kuabudu |
|---|---|---|
| **2 Mambo ya Nyakati 7:14 -** *kama watu wangu, wanaoitwa kwa Jina langu, watajinyenyekesha na kuomba na kuutafuta uso wangu na kuacha njia zao mbaya, basi nitasikia toka mbinguni na kuwasamehe dhambi yao na nitaiponya nchi yao.*<br>● Tubu kwa niaba ya uongozi na watu wote wa Kenya kwa maovu ambayo yametokea katika nchi.<br>● Mwombe Bwana Yesu atusaidie kuomba, kuutafuta uso wake na kuacha njia zetu mbaya, ili atusamehe dhambi zetu na kuliponya taifa.<br>● Tubu kwa niaba ya uongozi na watu wote wa Kenya kwa ufisadi katika kila sekta ya taifa hili. Ungama kwa Bwana Yesu na utubu nyakati zote ambazo watu wake wameshiriki katika ufisadi.<br>● Tubu kwa niaba ya uongozi na watu wote wa Kenya kwa ajili ya damu iliyomwagika.<br>● Tubu kwa jinsi tulivyoharibu mazingira yetu na kufanya mambo ambayo yamekuwa na athari mbaya kama vile mafuriko, majengo yanayoporomoka, gharama kubwa ya maisha, n.k.<br>● Omba Mungu awafariji na kuleta urejesho kwa watu wote waliopoteza wapendwa wao na mali kutokana na mafuriko, majengo yaliyoporomoka, nk.<br>● Ombea njia ya kimungu katika sekta ya afya na elimu.<br>● Omba Mungu aingilie kati uchumi na nyakati ngumu za kiuchumi zinazowakabili wengi.<br>● Ombea uamsho wa kitaifa na uponyaji wa kiroho. | **Matendo 17:26-27 -** *Yeye aliumba mataifa yote ya wanadamu waishi juu ya nchi kutokana na mtu mmoja. Pia amepanga muda wa maisha ya watu wote, akaweka na mipaka ya mahali watakapoishi ili wamtafute Mungu na wamfahamu. Lakini Yeye hayuko mbali nasi.*<br>● Mshukuru Mungu kwamba ndiye aliyeamua kwamba Kenya itakuwa taifa katika wakati huu wa historia.<br>● Tangaza utukufu wa Mungu, nuru, uwepo, amani, baraka, na utawala juu ya Kenya.<br>● Omba Wakenya wamtafute Mungu na kwamba makusudi yake na mipango yake itatawala katika taifa hili.<br>● Ombea viongozi wote wa Kenya hekima na uadilifu katika sekta zote, na katika kila ngazi ya uongozi, na kwamba mioyo yao itageukia Bwana Yesu kwa dhati na kujisalimisha kwa ubwana wake.<br>● Ombea sekta zote za uchumi zistawi - biashara, kilimo, utalii, n.k., na zitawaliwe na kanuni za kimungu.<br>● Ombea suluhu bunifu na za kimungu kwa matatizo katika kila sekta nchini Kenya.<br>● Omba kwamba taifa la Kenya litaleta utukufu na sifa kwa Bwana Yesu na kuwavuta wengine kwa nuru yake. | **Zaburi 95:1-7 -** *Njooni, tumwimbie BWANA kwa furaha; tumfanyie kelele za shangwe Mwamba wa wokovu wetu. Tuje mbele zake kwa shukrani, tumtukuze kwa vinanda na nyimbo. Kwa kuwa BWANA ni Mungu mkuu, mfalme mkuu juu ya miungu yote. Mkononi mwake mna vilindi vya dunia, na vilele vya milima ni mali yake. Bahari ni yake, kwani ndiye aliifanya, na mikono yake iliumba nchi kavu. Njooni tusujudu, tumwabudu, tupige magoti mbele za Bwana Muumba wetu, kwa maana yeye ndiye Mungu wetu, na sisi ni watu wa malisho yake, kondoo chini ya utunzaji wake.*<br>**Zaburi 65:1-2 -** *Ee Mungu, sifa zakungojea katika Sayuni; kwako wewe nadhiri zetu zitatimizwa. Ewe usikiaye maombi, kwako wewe watu wote watakuja.*<br>● Njooni mbele za BWANA kwa shukrani, mtukuzeni kwa nyimbo.<br>● Mwabuduni BWANA kwa jinsi alivyo, yote aliyoyafanya, na yote atakayofanya.<br>● Mwabuduni BWANA, mshukuru kwa maana yeye ni Mungu wetu, na sisi tu watu wa malisho yake, kondoo chini ya ulinzi wake.<br>● Tumwabudu BWANA kwa shauku, kwa maana yeye ni Mwamba wa wokovu wetu, aliye-tubeba kwa siku 21 za maombi na kufunga.<br>● Mshukuruni na kumsifu BWANA, kwa kuwa ametusikia tulipokuwa tukiomba.<br>● Mshukuruni na kumsifu BWANA, kwa maana yeye ndiye Mungu anayejibu maombi. |